**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU BUSTANI**

Simu Nambari**: 255-26-2360033**

E-MailNo**.** **bustanitc@gmail.com**

**Mobile No. 0758900881**
**0692063663**
**0743133331**

Chuo cha Ualimu Bustani,
S.L.P. 131,
**KONDOA.**

**NDG: ……………………………………..**

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA ELIMU MSINGI MCHEPUO WA SAYANSI YA JAMII KWA KISWAHILI, MWAKA WA MASOMO 2025/2026</u>**

## 1. UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukuarifu rasmi kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada ya Ualimu katika Chuo Cha Ualimu Bustani. Chuo kina dhamira ya kuwa kituo cha kuibua na kuendeleza stadi za Ualimu kwa kujikita katika maeneo ya Sayansi na Technolojia, Sayansi Asilia (Natural Science), masomo ya Ualimu, ujasiliamali na stadi za maisha ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji nchini. Hivyo unapaswa kuthamini uchaguzi huu kwa kusoma kwa bidii, kufuata taratibu na kanuni za Chuo ili uweze kufikia malengo yako binafsi na malengo ya Taifa kwa ujumla.

## 2. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo cha Ualimu **Bustani** kipo Mkoa wa **Dodoma,** Wilaya ya **Kondoa**. Kipo kilometa 3.5 kutoka standi kuu ya magari (**Bicha**) au kilometa 2 kutoka stendi ya mabasi Kondoa mjini

## 3. TAREHE YA KURIPOTI CHUONI

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe ________________na tarehe ya mwisho kuripoti ni tarehe _______________bila kukosa ili kuanza mafunzo. Iwapo hutafika chuoni mpaka tarehe ________________ hutapokelewa. Mara baada ya kuwasili Chuoni fika ofisi ya usajili ambapo utapokelewa na kupewa maelekezo. Mwanachuo haruhusiwi kwenda bwenini au maeneo mengine ya chuo kabla ya kusajiliwa. Ili uweze kusajiliwa unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo:

- Fomu ya maelekezo ya kujiunga na Chuo (Joining instruction).
- Cheti halisi cha matokeo ya kidato cha nne na nakala yake.
- Cheti halisi cha matokeo ya kidato cha sita na nakala yake.
- Hati ya matokeo ya kidato cha sita (Result slip) kwa wale waliohitimu kidato cha sita Mei 2025 (na nakala zake)
- Cheti halisi cha Ualimu ngazi ya Astashahada (Daraja la tatu A) na nakala yake.
- Cheti halisi cha kuzaliwa na nakala yake.
- Cheti cha kumaliza kidato cha sita (Leaving certificate)
- Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
- Risiti za malipo ya michango (Original bank pay in-slip)
- Bahasha (A4) na nakala za vyeti

**N.B Hautapokelewa wala kusajiliwa usiporipoti na mahitaji haya**

## 4. VIFAA VINAVYOHITAJIKA

### a. Vifaa vya malazi

Mashuka mawili rangi ya blue bahari, blanketi 1, mto 1, chandarua nyeupe 1 na foronya 2 za blue bahari.

### b. Vifaa vya chakula

Vyombo vya kulia chakula (sahani 1, kikombe 1, bakuli 1, kijiko 1) galoni ya lita tano ya plastiki kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa yaliyochemshwa, pamoja na ndoo moja ya lita kumi kwa ajili ya kuogea

### c. Vifaa vya michezo

Nguo za michezo (bukta na T-shirt rangi yoyote pamoja na raba jozi moja ya rangi yoyote, track suti rangi ya **Blue bahari** kwa ajili ya mchakamchaka na jogging siku za Jumamosi na ziara za kimichezo.

### d. Vifaa vya taaluma.

- Daftari zisizopungua **15 QUIRE 3**, kalamu za wino, mkebe wa Hisabati.
- Unatakiwa kuja na muhtasari wa masomo ya shule za msingi na kozi uliyochaguliwa.
- Karatasi **Rimu 1 (A4**)

## 5. ADA YA CHUO

Ada ya mafunzo ni **Tsh 450,000/=** kwa mwaka, au unatakiwa kulipa kiasi kisichopungua **Tsh 225,000/= kwa** muhula. Fedha hiyo unapaswa kuingiza kwenye simu ya mtandao wowote na utapata maelekezo ya namna ya kulipa ada kwa kutumia **control** number ukifika Chuoni. Mwanachuo hatasajiliwa ikiwa atakosa ada.

## 6. MICHANGO YA CHUO

Mbali na fedha hiyo utatakiwa kutoa michango katika maeneo yafuatayo

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Ulinzi | 30,000/= kwa mwaka |
| 2 | Ukarabati | 25,000/= kwa mwaka |
| 3 | Usafi na Mazingira | 20,000 kwa mwaka |
| 4 | Huduma ya kwanza | 10,000/= kwa mwaka |
| 5 | Michezo | 30,000/= kwa mwaka |
| 6 | Kukodi godoro | 10,000/= kwa mwaka |
| 7 | Usajili | 20,000/= kwa mwaka |
| 8 | Mchango wa serikali ya wanachuo | 5,000/= kwa mwaka |
| 9 | Mchango wa bima ya afya **(NHIF)** | 50,400/= **kwa asiyekuwa nayo** |
| | **JUMLA KUU** | **200,400/=** |

Jumla ya michango ya Chuo Tsh **195,400**/= kwa mwaka ziwekwe kwenye account namba **50201100020 (NMB) (BUSTANI TEACHERS' COLLEGE FUND**) bila kukosa

Mchango wa serikali ya wanachuo **5,000/=** iwekwe kwenye account namba **50210010117 (NMB) (BUSTANI STUDENT ORGANISATION).**

**N.B.** Wasilisha risiti za malipo ya bank kwa msajili ukifika Chuoni. Aidha **usije** na fedha tasilimu chuoni. **Usichanganye** akaunti kwani fedha ikilipwa kimakosa hairudishwi

## 7. MAVAZI

Mavazi yatakayovaliwa na mwanachuo wakati wote Chuoni SHARTI yawe ya HESHIMA, SAFI na yenye kuendana na masharti kwenye Kanuni hizi.

Mwanachuo analazimika kuvaa sare kamili ya Chuo wakati wote na mahali popote (ndani na nje ya chuo) katika kipindi chote cha masomo (semista/muhula); isipokuwa wakati wa kazi za nje, nyakati za jioni baada ya masomo, au siku za mapumziko ndani ya chuo.

Mwanachuo anatakiwa kuvaa kitambulisho chake shingoni wakati wote awapo chuoni au nje ya chuo kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma.

**a. Sare kwa wanaume:**

i. Suruali ya bluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up). Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na suruali linaweza kuvaliwa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.

ii. Shati liwe bluu bahari (light blue) mikono mirefu.

iii. Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) na nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali.

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi.

v. Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno (mlegezo)

vi. Uvaaji wa jinzi, kaptula, bangili, cheni, vimodo, skafu, makobazi, na pete (zisizo za ndoa) hauruhusiwi.

vii. Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni T- shirt nyeupe na track suit ya bluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.

viii. Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kupasua kuni, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua. Kujirudia kwa makosa kutapelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo, kupewa kazi ngumu na, auataachishwa mafunzo.

**b. Sare kwa wanawake:**

i. Sketi rinda boksi ya buluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenye urefu unaozidi magoti na zisizobana. Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi linaweza kuvaliwa.

ii. Shati iwe light blue mikono mirefu na tai ndefu dark blue na nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi.

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi, na soksi ndefu nyeupe.

iv. Nywele zichanwe au zisukwe mtindo wa utii wa roda mistari mitano hadi nane au kubana kisogoni kwa kibanio cheusi.

v. Uvaaji wa nguo angavu, khanga, kitenge, suruali, kofia, kilemba, hereni, bangili, mkufu, shanga, pensi, miniskirt, 88 nguo zenye mpasuo unaozidi magoti, makobazi na pete (isipokuwa pete ya ndoa) hauruhusiwi.

vi. Mwanachuo atakayependa kujisitiri kwa vazi la hijab anaelekezwa kumwona mlezi wake wa kike kwa maelekezo bayana.


vii. 6Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni T- shirt nyeupe na track suit ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.


viii. Uvaaji wa mavazi yasiyokubalika kwa kuvunja kanuni utapelekea mavazi hayo kuchukuliwa na kuhifadhiwa ofisi ya msajili na kufuatiwa na adhabu ya papo kwa papo. Mavazi yaliyoshikiliwa yatarejeshwa kwa mwanachuo atakapomaliza mafunzo.

ix. Mwanachuo atakayeenenda kinyume na kanuni yoyote kati ya kanuni atastahili adhabu ya papo kwa papo ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba moramu/kifusi, kuchimba shimo la taka, kupasua kuni, kuchimba kisiki, kuchimba mtaro, kuotesha miti/maua. Kujirudia kwa makosa kutapelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo, kupewa kazi ngumu na, auataachishwa mafunzo.

**MUHIMU:**

i. Ilikupata mfanano wa sare za chuo na zinazokubalika unashauriwa kupata maelekezo ya kina kutoka chuoni kabla ya kushona au kununua
ii. Kila mwanachuo anapaswa kuwa na T-Shirt ya blue bahari yenye nembo ya chuo inayopatikana chuoni kwa gharama ya Tsh 20,000/=. Fedha hiyo iwekwe kwenye akauti namba **50210010117 (NMB) (BUSTANI STUDENT ORGANISATION).**
iii. Kila mwanachuo atatakiwa kuchangia gharama ya mahafali kiasi cha Tsh10,000/= kwa mwaka
iv. Fedha hiyo iwekwe kwenye akauti namba **50201100020 (NMB) (BUSTANI TEACHERS' COLLEGE FUND**)





**MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA WANACHUO**

i. Mwanachuo anashauriwa aje na fedha tasilimu kwa ajili ya matumizi binafsi.
ii. Mwanachuo mwenye kadi ya bima ya afya ni muhimu kuja nayo.
iii. Mwanachuo atapaswa kufanya uchunguzi wa afya katika Hospitali za wilaya au mikoa kwa kutumia fomu iliyoambatanishwa hapo chini.

**8. CHAKULA**

i. Chuo kinatoa chakula kwa mujibu wa miongozo ya serikali.
ii. Chuo hakitoi chakula maalum (**special diet**) kwa wanachuo wenye mahitaji hayo

**9. SHUGHULI ZA UZALISHAJI MALI CHUONI**

Ili kutekeleza mtaala wa mafunzo ya **Elimu ya Ualimu** kwa ufanisi chuo kinaendesha shughuli za kilimo hususani mazao ya bustani na ufugaji. Lengo kuu ni kuwafanya wanachuo wajifunze kwa nadharia na vitendo katika masomo yao hususani stadi za maisha, ili kutekeleza mtaala wa **Ualimu ambao unazingatia falsafa ya elimu ya kujitegemea unatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo; Jembe-kila mwanachuo, Reki – wavulana tu, Fagio ndefu za chelewa (chelewa kubwa) – wasichana tu.** Ili kuendeleza utoaji wa huduma katika maeneo hayo kutakuwa na utaratibu wa kubaki chuoni wanachuo kwa zamu angalau mara moja kwa kipindi chote cha mafunzo wakati wa likizo kwa lengo la kuendeleza utoaji wa huduma katika bustani, mifugo na mazingira ya chuo kwa ujumla.

**10. MWISHO**


Jumuiya ya chuo cha Ualimu Bustani inakutakia maandalizi mema ya safari ya kuja chuoni.

**KARIBU SANA**



JOYNA ELISHA CHANAFI

**MKUU WA CHUO**




**NAKALA:**

i. Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S. L. P 10,
**DODOMA.**

ii. Mkurugenzi Mafunzo ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S. L. P 10`,
**DODOMA.**

iii. Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule,
Kanda ya Kati,
**DODOMA**

(iv) Afisa Elimu (M),
**DODOMA**

(v) Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo,
Chuo cha Ualimu Bustani

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA MWENENDO BORA WA MWANACHUO

Tabia na mwenendo wa mwalimu ni mfano wa kuigwa kwa wanachuo wake na jumuiya anamoishi. Maneno yake na matendo yake, vyote viwe mifano mizuri inayofaa kuigwa. Kwa kuwa ualimu bora huanzia chuoni, kazi moja kubwa ya Chuo cha Ualimu ni kuwasaidia wanachuo kuwa na haiba ya ualimu. Haiba ya mwanachuo hujengwa. Kwa hiyo, kuwa na mwenendo bora husaidia kuwafanya waishi kwa usalama, amani, matumaini, heshima na mafanikio. Utekelezaji wa kanuni na taratibu utategemea hali ya mazingira ya Chuo. Kwa hiyo, kila Chuo hakina budi kuwa na kanuni bora zinazohusu afya, mavazi, heshima, utii, usafi, chakula, kazi, masomo, ruhusa na sheria za nchi kama ilivyofafanuliwa:

**a. Afya**

i. Kabla ya kusajiliwa, kila mwanachuo lazima apimwe afya na awe na cheti cha daktari wa Serikali kinachoonesha kwamba afya yake ni nzuri kwa ajili ya Mafunzo ya Ualimu;

ii. Mwanachuo mwenye mimba au atakayempa mimba mwenzake wakiwa mafunzoni watalazimika kuahirisha Mafunzo ya Ualimu;

iii. Mwanachuo aliyetoa mimba au anayejaribu kutoa mimba ataondolewa chuoni kabisa;

iv. Mwanachuo haruhusiwi kutumia pombe, bangi, sigara au madawa ya kulevya.

**b. Mavazi**

i. Mwanachuo anapaswa kuvaa sare wakati wa vipindi na akiwa nje ya Chuo;

ii. Mwanachuo haruhusiwi kuvaa sare za Chuo au nguo za kawaida zilizochakaa, zinazobana au zilizochafuka;

iii. Mwanachuo anapaswa kuwa na sare maalumu za michezo na zivaliwe wakati wa michezo; na

iv. Mwanachuo atatakiwa kuvaa mavazi nadhifu na yenye staha muda wote.

**c. Heshima na Utii**

i. Mwanachuo anapaswa kujiheshimu na kuwa na lugha yenye hadhi ya ualimu, na matendo yake yawe yanakuza heshima yake;

ii. Mwanachuo awaheshimu wenzake, wafanyakazi wa Chuo na watu wengine anaokutana nao;

iii. Mwanachuo haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mkufunzi au mfanyakazi mwingine pasipo ruhusa maalumu;

iv. Mwanachuo wa kike haruhusiwi kwenda kwenye bweni la wavulana au mvulana kwenda kwenye bweni la wasichana isipokuwa kwa kibali maalumu cha Mratibu wa Masuala ya Wanachuo;

v. Wanachuo wa kike na wa kiume wanapaswa kuishi kama kaka na dada. Hivyo, ni makosa kuonesha kwa njia yoyote ile kwamba wanaishi kama mtu na mpenzi wake;

vi. Mwanachuo haruhusiwi kuwa na tabia ya uasherati, usagaji, ushoga, ubakaji, unajisi au uzinzi na mtu yeyote yule;

vii. Mwanachuo sharti awahi mahali popote anapohitajika kama vile mstarini, bwaloni, ukumbini, darasani, katika kazi za nje na anapoitwa kwa kengele au ishara zingine; na

viii. Mwanachuo haruhusiwi kutoa au kusambaza taarifa za uongo, kufitini, kuzusha mambo yanayoweza kuleta taharuki na kuvunja amani chuoni.

**d. Usafi**

i. Mwanachuo anapaswa kuzingatia usafi wa mwili, ikiwa ni pamoja na kuwa na nywele fupi, kukata kucha na kunyoa ndevu;

ii. Mwanachuo anatakiwa kuweka sehemu yake ya malazi katika hali ya usafi muda wote;

iii. Mwanachuo anapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli za nje na ndani ya darasa.

**e. Kazi**

i. Mwanachuo anapaswa kufanya kazi anazopewa kwa ufanisi na hatakiwi kuacha kazi aliyopewa bila ruhusa; na

ii. Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufanya kazi za mikono kwa weledi.

**f. Masomo**

i. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo na vya kujisomea kwa mujibu wa ratiba ya Chuo;

ii. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria na kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote inayotolewa;

iii. Mwanachuo anapaswa kufaulu mazoezi, majaribio na mitihani inayofanywa kulingana na kiwango kilichowekwa;
iv. Mwanachuo anapaswa kujiandaa vizuri na kufanya mazoezi ya kufundisha kwa muda na kwa utaratibu uliopangwa; na
v. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria darasani siku zote za masomo kulingana na muhula husika.

**f. Mali na Vifaa**

i. Mwanachuo haruhusiwi kuiba, kuharibu, kuchafua majengo au kupoteza mali ya umma au ya Chuo au ya watu wengine;
ii. Mwanachuo ana wajibu wa kulinda na kutunza mali yake binafsi, za wanachuo wenzake na mali ya umma;
iii. Mwanachuo anapaswa kujiepusha na vitendo vya ubadhirifu na ufujaji wa mali ya umma kama vile maji na umeme;
iv. Mwanachuo anapaswa kutunza na kurejesha kwa wakati vifaa anavyoazima au kukabidhiwa kama vile vitabu, vifaa vya darasani, bwaloni na bwenini; na
v. Mwanachuo anapaswa kuzingatia matumizi sahihi ya vifaa vya mawasiliano kwa kufuata sheria na taratibu za Chuo na nchi.

**g. Ruhusa**

i. Mwanachuo anapaswa kuomba ruhusa kila anapotoka nje ya Chuo;
ii. Kutakuwa na muda maalumu wa kuitisha majina ambao kila mwanachuo lazima ahudhurie kwa utaratibu utakaopangwa na Chuo;
iii. Mwanachuo haruhusiwi kutembelea nyumba za starehe, wageni na vilabu vya pombe; na
iv. Mwanachuo haruhusiwi kumkaribisha mgeni katika mazingira ya Chuo bila kibali.

**h. Sheria za Nchi**

i. Mwanachuo anapaswa kufuata maagizo na sheria za nchi;
ii. Mwanachuo anapaswa kuwa na heshima kwa viongozi wa Serikali;
iii. Mwanachuo anapaswa kuheshimu alama za Taifa, ikiwa ni pamoja na Bendera, Wimbo na Nembo ya Taifa (Ngao ya Taifa)
iv. Ni kosa kwa mwanachuo kutumia nafasi au uwezo wake kufanya wenzake ama watu wengine wasitii Serikali halali ya nchi au chombo chochote halali cha Serikali; na

v. Mwanachuo anapaswa kuzifahamu na kuzifuata kanuni, taratibu na mwenendo mwema wa maadili ya ualimu.

**ZINGATIO**

Unataarifiwa kuwa chuo hiki ni cha Serikali wala siyo cha DINI. Hivyo kinazingatia katiba ya nchi kuhusu

uhuru wa kuabudu, kila mwanachuo huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao. Pia kuwa na vipindi vya dini katika ratiba za masomo.

Wanachuo hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba ya chuo au baada ya vipindi tofauti na ratiba iliyowekwa

**KUWA MWALIMU BORA NA MWENYE MAADILI INAWEZEKANA**

**TIMIZA WAJIBU WAKO**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU BUSTANI**

Simu Nambari**: 255-26-2360033**
E-MailNo**.** bustanitc@gmail.com

Mobile No. 0758 900881
0692 063663
0743 133331

Chuo cha Ualimu Bustani,
S.L.P. 131,
**KONDOA.**

26/07/2024

Mimi ……………………………………………………………………………………………………
Niliye chaguliwa kujiunga na CHUO CHA UALIMU BUSTANI mwaka 2022/2023 nimesoma maelekezo ya kujiunga na chuo pamoja na sheria na taratibu za Chuo hivyo ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yangu binafsi, Malengo ya Chuo na Taifa kwa ujumla.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu na nyeti kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika mafunzo yangu nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajila yangu pia. Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa chuoni:

1. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu kama Mwalimu tarajali
2. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za chuo kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazo tolewa mara kwa mara na uongozi wa Chuo
3. Sitajihusiha na vitendo vya utovu wa nidhamu katika muda wote wa mafunzo
4. Nitakubali kupewa huduma stahiki kama chakula kulingana na taratibu na uwezo wa Chuo
5. Nitashiriki katika shughuli zote za nje ya darasa kwa moyo wa kizalendo ili kukitumikia chuo na taifa langu.
6. Ikiwa nitakikiuka kiapo hiki pamoja na kanuni na taratibu za chuo kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/mlezi

wangu…………………………………………………………………………(Jina la Mzazi/Mlezi) kwa ajili ya hatua zaidi na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayotolewa na Kamati ya nidhamu ya Chuo kwa mujibu wa sharia na taratibu za chuo.

Saini ya Mwanafunzi…………………………………………Tarehe……………………………………………

***SEHEMU YA MZAZI/MLEZI***

Mimi……………………………………………………………………………………………………..
ninakubali
kupokea nafasi yakijana wangu (jina)…………………………………………..kujiunga katika Chuo cha Ualimu Bustani mwaka 2024. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya chuo kwa wakati kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na chuo. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Chuo kwa kulipa michango kwa wakati ili kumwezesha mwanangu kutekeleza wajibu wake kwa chuo na Taifa kwa ujumla

Anuani yangu ya kudumu, S.L.P……………………………………………………………………...
Wilaya ………………………………………………………………..
Mkoa ………………………………………………….
Makazi…………………………………………………………………….
Shughuli/kazi…………………………………………………………………

Simu……………………………………………………………………………….
Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nitajulisha Chuo kwa maandishi ili kurahisisha mawasiliano

Saini: Mzazi/Mlezi…………………………….…………

Tarehe…………………………..……

## GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO: The Medical Officer,

**PART A:**

Please examine

Mr/Mrs/Miss………………………………………………………………………………..

To his/her physical and mental fitness for a full time a part time vocational course.

A: 1. (i) Eye – sight

(ii) Hearing

(iii) Speech

(iv) Venereal Diseases

(v) Leprosy

(vi) Limbs

(vii) Epilepsy

2. Neuroses

3. Other serious diseases. B: Blood Group

Date: ……………………. Signature………………Official Stamp……………………………

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above-named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a part time vocational course.

I. (a) Eye – sight…………………………………………………………
   (b) Hearing……………………………………………………………...
   (c) Limbs………………………………………………………………
   (d) Speech……………………………………………………………….
   (e) Leprosy……………………………………………………………….

II. Neuroses…………………………………………………………………

III. Other serious
   (a) Diseases……………………………………………………………..
   (b) Pregnancy……………………………………………………………

**Date: ……………………….. Signature………………… Official stamp......................................**